JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA KARAGWE**

*Unapojibu tafadhali taja;-*

Kumb.Na. HB.43/317/01/02 19/01/2026

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa kutuma maombi katika nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira ya Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe.

### A. SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe ni Raia wa Tanzania, mkazi wa Wilaya ya Karagwe.
ii. Awe na umri kuanzia miaka 55 hadi 65.
iii. Awe Mwadilifu.
iv. Awe na ufahamu katika mojawapo ya fani zifuatazo:-
- Menejimenti ya Rasilimaliwatu (Human Resource Management)
- Utawala wa Umma (Public Administration)
- Sheria (Law)

v. Awe Mstaafu Serikalini.
vi. Awe hajawahi kushtakiwa kwa kosa lolote la jinai.

### B. KAZI ZA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA

i. Kuendesha/Kuongoza vikao vya Usahili wa Waombaji wa nafasi za kazi.
ii. Kuendesha/Kuongoza vikao vya kuthibitisha kazini watumishi pamoja na kuwapandisha/kuwabadilisha watumishi vyeo.

### C. POSHO

Kazi hii haina mshahara wa kila mwezi. Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atakuwa analipwa posho kutokana na vikao vitakavyo kaliwa na Bodi.

### D. MAELEKEZO/MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.

1. Waombaji wote watume barua za maombi zikiwa na viambata vifuatavyo:-



CamScanner

## D. MAELEKEZO/MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.

1. Waombaji wote watume barua za maombi zikiwa na viambata vifuatavyo:-
   i. Cheti cha kuzaliwa, pamoja na vyeti vya kitaaluma yaani Kidato cha nne, Kidato cha Sita, Stashahada ya Juu au Shahada vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.
   ii. Wasifu au maelezo binafsi yaliyojitoleza (Detailed Curriculum Vitae), yenye anuani inayotumika, namba za simu, anuani ya barua pepe(Email Address), pamoja na wadhamini (Referees) watatu na kuaminika.
   iii. Barua ya utambulisho kutoka kwa Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa.
   iv. Picha mbili (2) za pasipoti za hivi karibuni.
   v. Wasifu Binafsi (CV)
   vi. Barua toka kwa wadhamini wawili (2) zikiwa na anuani kamili.
2. Maombi yatumwe kuanzia tarehe **19/01/2026 hadi tarehe 02/02/2026.**
3. Barua zote za maombi zitumwe kupitia Posta kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya,
01Barabara ya Ikulu,
S.L.P 20,
<u>35482 KARAGWE.</u>

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA :**

H.J. Msanga,
**<u>MKURUGENZI MTENDAJI (W).</u>**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KARAGWE

**Nakala:** Katibu Tawala (M),
4Barabara Luhangisa,
S.L.P 299,
<u>3511-BUKOBA</u>

<u>NB</u>;-*Tangazo hili ni la Marudio ya Tangazo lenye* ***Kumb.Na. HB.43/317/01/01*** *la tarehe* ***30/12/2025.***



CamScanner